**ZIARA YA MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO PAMOJA NA WATAALAMU WAKE KUANZIA TAREHE 18-21 MWEZI APRILI, 2017.**

## KATA YA MIGAMBO: 18/4/2017

### Kijiji cha Kwefingo: Kukabidhi dume bora la ng'ombe

Kikundi cha akina mama wajane kilichopo katika kitongoji cha Milungui katika kijiji cha Kwefingo kilichopo katika kata ya Migambo kilianza mnamo mwaka 2006 kikiwa na wanachama 30. Kwa sasa wapo 15 na kikundi hicho kinaitwa UMOJA group.



*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto akikabidhi dume bora la ng'ombe kwa kikundi cha akina mama wajane waliopo katika kata ya Migambo,kijiji cha Kwefingo.(Picha na ofisi ya Mipango)*

Dume namba 35087 jina lake ni LOY aina ya freshian lilikabidhiwa kwa kikundi cha UMOJA group.Wanachama hao wa kikundi cha UMOJA group walimuomba Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto awapatie kuku wa kufuga ili wakuze kipato chao.

AHADI ZA MKURUGENZI MTENDAJI

- Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto Mh.Kazimbaya Makwega alikubali ombi la wanakikundi cha UMOJA kwamba atawapatia majogoo bora ya kuku ili waweze kufuga kwa tija ila sharti wanakikundi hao wajenge mabanda bora ya kufugia kuku ndipo ahadi hiyo itatekelezwa.Wanakikundi cha UMOJA wameahidi kujenga mabanda bora ya kuku kabla ya tarehe 30/7/2017.

KATA YA RANGWI

Kijiji cha Kisirui: Kukabidhi dume bora la ng'ombe

Kikundi cha ufugaji wa ng'ombe kilichopo katika kijiji cha Kisirui kinachojulikana kama SONGAMBELE kimepatiwa dume bora la ng'ombe na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto.Kikundi kimekabidhiwa dume bora la ng'ombe namba 35083 linalojilikana kwa jina la Balozi.





*Picha namba moja juu, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto,Mh.Kazimbaya Makwega kikagua kitalu cha kuoteshea miti cha kikundi cha ufugaji kilichopo katika kijiji cha Kisirui,kata ya Rangwi.Picha namba mbili chini,Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto akikabidhi mkataba wa makabidhiano ya dume bora la ng'ombe kwa mmoja wa wanakikundi cha ufugaji katika kijiji cha Kisirui.(Picha na ofisi ya Mipango).*

Katika ziara hiyo iliyofanyika kwenye kijiji cha Kisirui, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto alitembelea Shule ya msingi Kisirui ambayo ni Shule mpya ambayo tayari ina madarasa mawili yaliyokamilika.Uongozi wa kijiji hicho upo katika hatua za kuongeza madarasa mawili na kwa sasa wapo katika levo ya msingi.

AHADI ZA MKURUGENZI MTENDAJI

- Mkurugenzi ameahidi kutoa bati na saruji mifuko 25 ili kufanikisha ujenzi wa madarasa hayo mawili na ofisi ya mwalimu.Ahadi ya kutoa bati pamoja na saruji itatolewa mnamo tarehe 2 Mwezi Mei mwaka 2017
- Mkurugenzi amemuagiza mtendaji wa kijiji cha Kisirui kuhakikisha wanatafuta namna ya kuongeza darasa jingine la tatu ili kupunguza uhaba wa vyumba vya madarasa katika shule hiyo.Pia wananchi wametakiwa kuchangia nguvu zao pamoja na kusomba mawe ili kufanikisha ujenzi huo.
- Mkurugenzi amewaagiza wanakikundi cha ufugaji Kisirui kumtunza dume huyo ili awapatie mafanikio
- Vilevile Mkurugenzi Mtendaji ameahidi kuwapa kilo tano (5) za mbegu za miti aina ya pine kwa wanakikundi cha ufugaji cha Kisirui kwa kuwa pia wanajihusisha na uoteshaji na upandaji wa miti.

Kijiji cha Emao: Kukabidhi dume bora la ng’ombe

Dume namba 35088 aina ya freshian ameshakabidhiwa kwa kikundi cha wafugaji cha Emao.Naye Diwani wa viti Maalum katika kata ya Rangwi Mh.Marietha alimshukuru Mkurugenzi Mtendaji kwa msaada wa dume bora la ng’ombe kwani litawasaidia wananchi wake kujikwamua kiuchumi.

KUSHIRIKI KLINIKI TEMBEZI

Kliniki tembezi ni zoezi la kibunifu linalolenga kusogeza karibu huduma za afya kwa wananchi ambapo watabibu kutoka Hospitali ya Wilaya walihusika kutoa huduma hizo bure kwa wananchi wa kipato cha chini.Zoezi hili lilifanyika katika zahanati ya Kisirui.

MAELEKEZO/AHADI ZA MKURUGENZI MTENDAJI

- Wananchi wameomba Mkurugenzi Mtendaji awasaidie kutatua kero ya maji ambapo Mkurugenzi ameeleza kuwa tayari Halmashauri ina mpango wa kupeleka

mabomba rola nane (8) na kupeleka katika kata ya Rangwi ila sharti wananchi wachangie nguvu zao katika kuchimba mitaro ya kupitishia bomba hizo.

- Kuhusu suala la kukosekana kwa nishati ya umeme kwa baadhi ya maeneo ya kata ya Rangwi Mkurugenzi ameahidi kuzungumza na Mbunge wa Jimbo la Mlalo ili aweze kusaidia kuhusu suala hilo ila alidokeza kuwa suala la umeme kupitia mpango wa kusambaza umeme vijijini (REA) lipo mbioni kufikia maeneo hayo.



*Picha ya juu, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto Kazimbaya Makwega akizungumza na wananchi wa kata ya Rangwi kwa kuwasikiliza kero zao ili kutafuta namna ya kuzitatua. Picha ya pili chini, Mkurugenzi Mtendaji akizindua zoezi la upimaji wa afya kwa wananchi wa kata ya Rangwi (kliniki tembezi) kwa kumpima mwanachi mmoja katika Zahanati ya Rangwi. (Picha na ofisi ya Mipango).*



## KIKAO NA WANAVIKOBA KATIKA KATA YA RANGWI

Mkurugenzi alifanya kikao na wanakikundi cha NYOTA NJEMA ambao wanajihusisha na VIKOBA na mpaka sasa kikundi hicho kina hisa ya Tshs 1,000,000/=.

MAELEKEZO/AHADI ZA MKURUGENZI MTENDAJI

- Mkurugenzi amewaagiza wanakikundi kufungua akaunti ya benki kwa ajili ya kuhifadhi fedha hiyo kwa usalama zaidi.Wameagizwa kufungua akaunti hiyo ya benki kabla ya siku ya Ijumaa tarehe 21/4/2017.
- Mkurugenzi ameahidi kuwapa Tshs 1,600,000/= wanakikundi cha VIKOBA cha NYOTA NJEMA kutoka katika fedha za akina mama na vijana kama 10% ya mapato ya ndani ya halmashauri inavyotakiwa kutumika kwa akina mama na vijana.Fedha hiyo ni ya mkopo kutoka Halmashauri na inatakiwa kurejeshwa ndani ya mwaka mmoja.

Kijiji cha Kiranga: Kukabidhi dume bora la ng’ombe

Kikundi cha UMOJA kilichopo katika kijiji cha Kiranga, kata ya Rangwi kilikabidhiwa dume bora la ng’ombe lenye namba 3650 aina ya freshian.Afisa Maendeleo ya jamii amewasihi wanakikundi kusajili kikundi chao katika ofisi ya maendeleo ya jamii ikiwa ni pamoja na ufunguzi wa akaunti benki.





*Mkurugenzi Mtendaji akimkabidhi mkataba wa makabidhiano ya dume bora la ng'ombe Mh.Diwani wa Kata ya Rangwi Mh.Omari Rashidi kwa ajili ya kikundi cha ufugaji katika kijiji cha Kiranga, picha ya chini, Mkurugenzi Mtendaji akikagua bwawa la samaki katika kijiji cha Kiranga, Kata ya Rangwi. (Picha na Ofisi ya Mipango).*

MAELEKEZO/AHADI ZA MKURUGENZI MTENDAJI

- Mkurugenzi amewaagiza wananchi kufungua akaunti benki na kuziweka fedha benki kisha halmashauri itawapatia kiasi sawa na kile walichoweka benki.Fedha hiyo itakuwa ni mkopo wenye riba ya 10% na itarejeshwa kwa muda wa mwaka mmoja.
- Afisa kilimo aliwasisitiza wananchi juu ya umuhimu wa kutumia vizuri chakula walichonacho na kuweza kuhifadhi chakula hicho.
- Kuhusu ufugaji wa samaki;Mkurugenzi ameahidi kuwapatia wanakikundi cha ufugaji wa samaki wavu wa kuvulia samaki ili waweze kuvuna samaki hao.
- Mh.Diwani wa kata ya Rangwi amemshukuru Mkurugenzi Mtendaji kwa msaada aliowapatia wananchi wa kata yake.

KATA YA MTAE

Kijiji cha Mtii:Kukabidhi vifaa vya kuhifadhia maziwa kwa kikundi cha uuzaji wa maziwa

Kikundi cha uuzaji wa maziwa katika kijiji cha Mtii kilikabidhiwa vifaa vitatu vya kuhifadhia maziwa (milk canes) kwa kikundi cha uuzaji wa maziwa katika kijiji cha Mtii.



*Mkurugenzi mtendaji akikabidhi vifaa vya kuhifadhia maziwa kwa kikundi cha ukusanyaji na uuzaji wa maziwa katika kata ya Kijiji cha Mtae, katika kata ya Mtae.(Picha na ofisi ya Mipango).*

Afisa maendeleo ya jamii aliwashauri wanakikundi cha uuzaji wa maziwa kusajili kikundi chao ili kitambuliwe na pia waweze kufungua akaunti benki.Mtendaji wa kata ya Mtae

aliahidi kukamilisha usajili wa kikundi hicho pamoja na kufungua akaunti ya benki kabla ya tarehe 5/5/2017.

Kijiji cha Mtii; kukabidhi dume bora la ng'ombe.

Kikundi cha JITEGEMEE kilichopo katika kijiji cha Mtii kilikabidhiwa dume bora la ng'ombe namba 35085.

MAELEKEZO/AHADI ZA MKURUGENZI MTENDAJI

- Mkurugenzi amewasihi wanakikundi cha ufugaji kumtunza vizuri ng'ombe huyo ili awapatie mafanikio
- Wafugaji wa ng'ombe wamemuomba Mkurugenzi Mtendaji kuwapatia bomba la kuogeshea wanyama wao na Mkurugenzi ameahidi kuwapatia bomba hilo,dawa pamoja na jiwe la kulamba wanyama
- Mkurugenzi ameahidi kuwapatia mbegu bora ya mbuzi (beberu) bali sharti ni kila mwanachama wa kikundi hicho awe anamiliki mbuzi jike watatu.
- Mkurugenzi pia ameahidi kuwapatia mbegu bora ya majogoo ya kuku kwa kila mwanachama mwenye matetea kumi atapata jogoo mmoja.
- Wanachama wote 13 wajitahidi kuwa na matetea kumi kila mwanakikundi mmoja.
- Pia Mkurugenzi amewataka wanachama hao wajenge mabanda bora kuku.Vilevile ameahidi kuwapatia dawa za kutibu magonjwa ya kuku.

KATA YA SHUME

Kijiji cha Gologolo : Kukabidhi kuku (majogoo bora)

Kijiji kimepewa kuku 15 ila bado mabanda ya kuku hwajajenga.Mkurugenzi amemuagiza mtendaji wa kijiji cha Gologolo pamoja na afisa ugani kuhakikisha wanawahimiza wananchi kujenga mabanda hayo haraka iwezekanavyo ili wanufaike na mradi huo wa kuku.

Kijiji cha Mkunki: Kugawa dume bora ng'ombe

Kikundi cha Umoja wa Wafugaji Mkunki (UWAM) kilikabidhiwa dume bora la ng'ombe namba 35084.Dume hilo la ng'ombe linaitwa Twitter.



*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto akikabidhi dume bora la ng'ombe kwenye kikundi cha ufugaji wa ng'ombe (UWAM) kilichopo katika kijiji cha Mkunki katika kata ya Shume.(Picha na ofisi ya Mipango).*

MAELEKEZO/AHADI ZA MKURUGENZI MTENDAJI

- Mkurugenzi ameahidi kuwapatia majogoo 23 kati ya watu 46; jogoo mmoja kwa kila wafugaji wawili.Sharti ni wafugaji hao kujenga mabanda kwa wakati.
- Mkurugenzi pia ameahidi kupeleka madume ya mbuzi katika kikundi hicho.Kila wanakikundi wawili watapewa bebeeru mmoja lakini sharti ni kila mwanachama awe na mbuzi jike watatu ndipo apewe mbuzi jike.
- Kuhusu suala la kukopeshwa mitamba (ng'ombe jike) Mkurugenzi ameahidi kulifanya kazi suala hilo ili kuona uwezekano wa kuwasaidia.
- Mkurugenzi pia ameahidi kuwapatia bomba la kupigia dawa/kuogeshea wanyama.

- Ifikapo tarehe 20/5/2017 masharti ya kununua mbuzi,kuku jike na kujenga banda ili wapatiwe mifugo hiyo kutoka Halmashauri.
- Kuhusu suala la kijiji cah Mkunki kutohudumiwa na TASAF , Mkurugenzi amejibu kuwa kijiji cha Mkunki hakipo miongoni mwa vijiji masikini na ndion maana hawapo katika mpango huo.
- Suala la vijiji kupatiwa Tshs milioni Hamsini kama ahadi ya Mh.Rais John Pombe Magufuli aliyoitoa wakati wa kampeni za kuwania kiti cha Urais mwaka 2015, Mkurugenzi ameeeleza kuwa suala hilo lipo mbionii kuanza katika vijiji mbalimbali nchini hivyo maandalizi ya kuunda vikundi yanatakiwa yaendelee ili fedha hiyo ikija waweze kunufaika nayo.
- Naye Afisa elimu amewahimiza wananchi wa Mkunki kuhakikisha watoto wao wanakula wakiwa shuleni ili waweze kusoma kwa utulivu na hivyo kuweza kuinua kiwango cha ufaulu.Pia amewasisitiza kumalizia ujenzi wa choo cha wanafunzi katika shule ya msingi Mkunki ili watoto wao waweze kukitumia na kuwaondolea adha wanayoipata.Choo hicho kinajengwa kupitia mradi wa SWASH.
- Mkurugenzi ameahidi kuliulizia suala hilo la ujenzi wa choo cha wanafunzi ifikapo Jumatano tarehe 26/4/2017 ambapo mratibu elimu kata ametakiwa ahakikishe kabla ya tarehe 25/4/2017 choo hicho kiwe kimekamilika na kutoa taarifa kwa Mkurugenzi Mtendaji.

KUSHIRIKI KLINIKI TEMBEZI KATIKA ZAHANATI YA KATA YA MANOLO

Mkurugenzi Mtendaji pamoja na timu yake walipata fursa ya kushiriki zoezi la kliniki tembezi (mobile clinic) ambapo zoezi hilo lilifanyika kwa mafanikio makubwa na wananchi walijitokeza kwa wingi.

20/4/2017

KUONGEA NA VIJANA KATIKA KATA YA MNG'ARO

Kikundi cha vijana wakulima kimetengewa jumla ya Tshs 10,000,000/= (milioni kumi) kwa ajili ya kufanya shughuli za kilimo cha vitunguu na Mkurugenzi amewapatia eneo la kiasi cha ekari 10 za kuanzia.





*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto akiwakabidhi vijana wa Kata ya Lunguza eneo la kufanya kilimo cha vitunguu; kikundi hicho cha ujasiriamali kitajumuisha vijana wawakilishi kutoka katika kata zote 33 za Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto. (Picha na Ofisi ya Mipango).*

MAELEKEZO/AHADI ZA MKURUGENZI MTENDAJI

- Mkurugenzi ameahidi kuwapatia vitambulisho vya bima ya afya (CHF) ili vijana hao waweze kupata huduma za afya kwa urahisi.Halmashauri itagharamia upatikanaji wa bima hizo (CHF)

Kijiji cha Kikumbi; Kukabidhi kuku

Agizo la kutengeneza mabanda ya kuku halikutekelezwa kwa kiwango kinachotakiwa.



*Mkurugenzi Mtendaji akimkabidhi kuku wa kufuga muuguzi wa zahanati ya kijiji cha Kikumbi ili kuwahamasisha wananchi wa Kikumbi kujiunga katika kikundi cha ufugaji.Picha ya juu, Mkurugenzi Mtendaji akikagua ujenzi wa banda la kufugia kuku uliofanywa na mwenyekiti wa kijiji cha Kikumbi.Katika mradi huo wa ugawaji wa majogoo bora kwa vikundi vya ujasiriamali, jumla ya majogoo 107 yaligawanywa katika mpango huo. Ndani ya kata mbalimbali za Halmashauri .(Picha na Ofisi ya Mipango).*

MAELEKEZO/AHADI ZA MKURUGENZI MTENDAJI

- Mkurugenzi amemuagiza mtendaji wa kata ya Mng'aro kutafuta kijiji kingine na shule moja nyingine nay eye atawapatia kuku wa kufuga (majogoo).Mkurugenzi ameahidi kupeleka kuku katika hicho kijiji kwa idadi ya kuku 100 na wanatakiwa kujenga mabanda kwa wakati.
- Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kikumbi ameagizwa kutengeneza banda mapema sana iwezekanavyo ili iwe mfano kwa wengine.
- Mkurugenzi ameahidi kumpatia mbegu mpya ya bata mwenyekiti wa kijiji cha cha kijiji Kikumbi ili aboreshe mifugo hiyo.
- Mkurugenzi ameahidi kumpatia bata mmoja wa kiume wa mbegu Mr.Hassan Mzinga wa Kikumbi ili aboreshe mifugo yake.
- Mkurugenzi amemkabidhi kuku wawili wa kiume (majogoo) muuguzi wa zahanati ya Kikumbi.Jumla ya majogoo 107 yamesambazwa katika vikundi mbalimbali vya ufugaji katika kata mabalimbali za Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto.
- Kuhusu kubomoka kwa sehemu ya kuwekea tanki la maji kwenye nyumba ya watumishi wa zahanati ya kikumbi, Mkurugenzi amemuagiza Mtendaji wa kijiji cha Kikumbi kurekebisha sehemu hiyo mwisho ni tarehe 28/4/2017.

KIKAO KIDOGO NA WANANCHI WA KIKUMBI:

Mkurugenzi alifanya kikao cha dharura na wanachi wa Kikumbi ili kuwaeleza umuhimu wa kutumia fursa mbalimbali wanazopewa na Serikali yao hususan kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto.

MAELEKEZO/AHADI ZA MKURUGENZI MTENDAJI

- Mkurugenzi amewahimiza wananchi wa Kikumbi kutekeleza maagizo wanayopewa na viongozi wao kwa wakati ili kuweza kujiletea maendeleo.
- Mkurugenzi ameahidi kutoa mbao kwa ajili kutengeneza shata za milango katika Shule ya Msingi Kikumbi ili madarasa yaweze kutumika vizuri ili wanafunzi wajifunze vizuri huku wakiwa wamekingwa na baridi.

KATA YA MBARAMO

Mkurugenzi Mtendaji alishiriki zoezi la kliniki tembezi katika zahanati ya kata ya Mbaramo ambapo wananchi walihamasika sana kuhudhuria kwa wingi kupata huduma hiyo ya bure.Mkurugenzi pia alifanya kikao na wanavikoba wa kata ya Mbaramo.





*Picha ya juu, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ,wa Kwanza upande wa kulia,akimsikiliza mmoja wa wanakikundi cha uuzaji wa sabuni katika kijiji cha Mbaramo.Picha ya pili chini, wanavikundi mbalimbali vya ujasiriamali ikiwemo VIKOBA wakimsikiliza kwa makini Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto.(Picha na Ofisi ya Mipango).*

| JINA LA KIKUNDI NA HISA ZAKE | | MAOMBI YA KIKUNDI | AHADI ZILIZOTOLEWA NA MKURUGENZI MTENDAJI |
|---|---|---|---|
| 1. | JITEGEMEE-Kikundi hiki kina jumla ya wanachama 30 na wanachama 7 ndio walihudhuria kikao hicho. | Kikundi kimeomba kupatiwa kuku kwa ajili ya kuanzisha mradi wa ufugaji wa kuku. | Mkurugenzi amewaagiza wanachama hao saba waliohudhuria kutafuta kuku 10 kwa kila mmoja kisha watapewa majogoo matatu kwa kila mmoja; sharti wawe wamejenga banda la kufugia kuku hao. |
| 2. | ZINDUKA-Kikundi hiki kina wanachama 30 na wanachama 8 walihudhuria kikao hicho.Kikundi hiki kina hisa ya jumla ya Tshs 1,800,000/= | Kikundi hiki kinajishughulisha na kilimo cha mboga mboga pamoja na kilimo cha tangawizi.Wamemuomba Mkurugenzi awapatie bomba la kupigia dawa, mbegu na dawa. | Mkurugenzi ameahidi kuwapatia msaada vifaa hivyo.Msaada huu wa kwanza unawahusu watu 8 waliohudhuria kikao tu. |
| 3. | UVIKI-Kikundi kina jumla ya wanachama 30 na wanachama 15 walihudhuria kikao hicho.Kikundi kina hisa ya jumla ya Tshs 3,500,000/= | Kikundi hiki kinajishughulisha na kilimo cha maharage na ufugaji wa mbuzi.Wanachama hawa wameomba kupatiwa dume bora la mbuzi. | Mkurugenzi amewaagiza wanakikundi cha UVIKI kutafuta majike ya mbuzi matatu kwa kila mmoja na ndipo Halmashauri itatoa dume moja moja kwa kila mwanachama kati ya 15 waliohudhuria.Mtendaji wa kata ametakiwa kufuatilia ujenzi wa mabanda bora ya kufugia kuku na mbuzi.Mkurugenzi amewapa wiki nane |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | (miezi miwili) ili kukamilisha maandalizi hayo. |
| 4. | CHAHIMBA-Kikundi kina jumla ya wanachama 30 na wanachama 6 tu walihudhuria.Kikundi hiki kina hisa ya Tshs milioni 7. | Kikundi hiki kinajihusisha na kilimo cha nyanya, pilipili ,karoti na hoho. | Mkurugenzi amewaagiza kununua mashine tatu za kumwagilia maji mashambani na Halmashauri itachangia nusu ya gharama ya kununulia mashine hizo na wao wenyewe watachangia nusu ya gharama.Bei ya mashine ni Tshs 500,000/=; wanakikundi watachangia nusu ya fedha hiyo na halmashauri itachangia nusu iliyobakia. |
| 5. | VIKAMBA-Kikundi hiki kina jumla ya wanachama 30 ila waliohudhuria ni wanachama 11.Kikundi hiki kina hisa yenye thamani ya Tshs 90,000/=. | Kikundi hiki kinajihusisha na ufugaji wa nyuki.Mpaka sasa kikundi kina mizinga 6 ya nyuki.Wameomba kupatiwa mizinga mingine ya nyuki ili wakuze mradi wao. | Mkurugenzi amewaagiza kila mwanachama achangie Tshs 35,000/= na Halmashauri itachangia Tshs 35,000/= kwa kila mmoja kwa wanachama hao 11 waliohudhuri ili kufikisha jumla ya Tshs 70,000/= kama fedha ya kununulia mzinga mmoja wa nyuki kwa kila mmoja. |
| 6. | Kikundi cha Mazingira Mbaramo-Kikundi hiki kina jumla ya wanachama 30 tu.Wanachama wanne | Kikundi kinajishughulisha na upandaji wa miti.Wamemuomba Mkurugenzi awapatie mbegu za miti aina ya | Mkurugenzi ameahidi kuwapatia vitu vyote walivyoomba isipokuwa itabidi kila mwanachama achangie kiasi cha Tshs |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | walihudhuria kikao hicho.Kikundi kina hisa ya Tshs 300,000/= | agricapus, pine msongoma pamoja na viriba na bomba la kunyweshea maji. | 5000/= kisha Halmashauri itaongeza fedha ili kununua mabomba 30 ya kunyweshea maji ( 30 water cans);moja kwa kila mwanachama. |
| 7. | NGUVU KAZI-Kikundi hiki kina wanachama 30 ila wanachama watano walihudhuria kwenye kikao.Kikundi kina jumla ya hisa yenye thamani ya Tshs 3,000,000/=. | Kikundi hiki kinajishughulisha na ufugaji wa kuku. | Mkurugenzi amewaagiza wanachama hao watano waliopo kununua matetea 15 kwa kila mmoja na baada ya hapo Halmashauri itampatia kila mmoja majogoo matatu.Pia wanachama hao watapatiwa dawa ya kideri pamoja na elimu ya ufugaji bora wa kuku. |
| 8. | UPENDO-Kikundi hiki kina jumla ya wanachama watano.Wanachama wane walihudhuria kikao.Kikundi hiki kina hisa ya Tshs 250,000/= mpaka sasa. | Kikundi hiki kinajishughulisha na uuzaji wa sabuni pamoja na kanga.Kwa sasa wameanza kulima zao la tangawizi.Mpaka sasa wamepanda kilo 5 za tangawizi.Wameomba kupatiwa mashine ya kunyweshea zao lao la tangawizi. | Mkurugenzi amemuagiza mtendaji wa kata kuhakiki ukweli wa kilimo kilimo hicho cha tangawizi.Bwana shamba pia ametakiwa kushiriki.Mkurugenzi ameamuagiza afisa maendeleo ya jamii kuwapatia Tshs 500,000/= kutoka katika fedha za akina mama ili wakuze mitaji yao. |
| 9. | WAHI-Kikundi kina wanachama 30 ila wanachama 4 walihudhuria kikao hicho. | Kikundi kinajihusisha na kilimo cha karanga.Pia wanajihusisha na kilimo cha ndizi.Wamemuomba Mkurugenzi Mtendaji | Mkurugenzi amewaagiza wanachama wa kikundi hicho kupanda migomba 15 kwa kila mmoja ndipo atawapatia mashine moja ya umwagiliaji ila |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | awasaidie mashine ya kumwagilia maji | watachangia nusu ya bei ya kununulia mashine hiyo. |
| 10. | CHAWAHI-Kikundi kina wanachama 30 ila wanachama wanne ndio walihudhuria kikao hicho. | Kikundi hiki kinajihusisha na ufugaji wa kuku na mpaka sasa wana hisa ya Tshs 2,000,000/=.Wana jumla ya kuku 15 mpaka sasa | Mkurugenzi amewaagiza kila mwanachama kati ya hao wanachama 30 ahakikishe anakuwa na matetea 15 na hapo kila mmoja atapewa jogoo mmoja. |
| 11. | JIHADIA-Kikundi kina wanachama 30. | Kikundi hiki kina hisa ya Tshs 1,500,000/=.Kikundi kinajihusisha na ununuaji wa tangawizi.Wameomba msaada wa kupatiwa mashine ya kumwagilia mazao yao. | Mkurugenzi amewaagiza kuwa na tabia ya kuazimana mashine zitakazokuwepo kwa kuwa wana mpango wa kuanzisha kilimo cha tangawizi |
| 12. | MSHIKAMANO-Kikundi kina jumla ya wanachama 30,mwanachama mmoja alihudhuria kikao. | Kikundi kinajihusisha na uuzaji wa mafuta ya kula.Kikundi kina hisa ya jumla ya Tshs 5,000,000/= | Mkurugenzi ameahidi kumpatia mbuzi dume mwanachama mmoja aliyehudhuria ila sharti awe amenunua mbuzi watatu wa kike ndipo ahadi hiyo itatekelezwa. |
| 13 | KIKUNDI CHA KILIMO UMBA-Kikundi kina watu 30.Wanachama wanne walihudhuria. | Kikundi kinajishughulisha na kilimo cha mboga mboga.Wameomba kupatiwa msaada wa mbegu za mazao ya mboga mboga. | Mkurugenzi ameahidi kuwapatia mbegu ya karoti na ngongwe.Wanachama wanne waliohudhuria na ndio watakaonufaika na msaada huo. |

Afisa mifugo amewashauri wananchi wa Mbaramo kutumia rasilimali zilizopo katika kutengeneza mabanda bora ya kuku na mbuzi.

Mh.Lucas Shemndolwa ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto aliweza kuhudhuria kikao cha wanavikundi wa VIKOBA wa kata ya Mbaramo ambapo alizungumza na wanavikoba wa kata ya Mbaramo kwa kuwasisitiza kufanya kazi kwa bidii na kutumia vizuri fursa mbalimbali zinazotolewa na serikali yao.



*Mh.Lucas Shemndolwa ambaye ndiye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya akishiriki zoezi la kliniki tembezi lililofanyika katika Zahanati ya Mbaramo,kata ya Mbaramo.(Picha na Ofisi ya Mipango).*

Pia Mh.Mwenyekiti amewasihi wananchi wa Mbaramo kupeleka watoto wao shule ili wapate elimu itakayowasaidia katika maisha yao ya baadae. Vilevile Mh.Mwenyekiti aliahidi kuwa ahadi zilizoahidiwa na serikali zinatekelezwa.Pia amewaagiza wataalamu kutoka Halmashauri kuandaa vijarida vidogo vyenye lugha rahisi ambavyo vitagawiwa kwa watu wanaoishi pembezoni ili waweze kujisomea na kuongeza ujuzi pamoja na uelewa wa mambo mbalimbali ya kijamii na kiuchumi.



*Mh.Lucas Shemndolwa ambaye ndiye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto akizungumza na wanajasiriamali wa Kata ya Mbaramo.(Picha na Ofisi ya Mipango).*